# EQUALITY FOR GROWTH (EFG)

# UKATILI WA KIJINSIA NA HAKI ZA WANAWAKE





Equality for Growth (EfG)

SAUTI YA MWANAMKE SOKONI

Equality for Growth (EfG)

**SAUTI YA MWANAMKE SOKONI**




# UKATILI WA KIJINSIA NA HAKI ZA WANAWAKE

UNITED NATIONS TRUST FUND TO END VIOLENCE AGAINST WOMEN

UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

## UTANGULIZI

Equality for Growth (EfG) ni shirika lisilo la kiserikali linaloendeleza usawa wa ukuaji kiuchumi, usawa wa kijinsia na kuwajengea uwezo wa kisheria na kibiashara wanawake walioko katika sekta isiyo rasmi nchini Tanzania. Shirika hili lilianzishwa mwaka 2008 likiwa na makao makuu yake Dar es Salaam.

## DIRA

Dira ya EfG ni kuona hakuna vikwazo vyovyote vya kijinsia kwa wanawake walio katika sekta isiyo rasmi na wanawake wakiwa mbali na aina zote za unyonyaji

## DHIMA

Dhima ya EfG ni kuinua maendeleo ya sekta isiyo rasmi Tanzania hususani wanawake kwa kupunguza umaskini kwa njia ya kutoa mafunzo ya haki za binadamu, msaada wa kisheria, kuwezesha kuwepo kuwepo kwa fursa sawa za kibiashara kwa wanawake, pamoja na kushawishi utungaji wa sera zinazoinua wanawake na kujenga uwezo kwa wanawake na wanaume.

## MALENGO

Kusaidia jamii ili kuona wanawake na wanaume wana haki na nafasi sawa ya kumiliki mali na shughuli za kiuchumi, utawala na kuinua maendeleo ya sera za uchumi na kijamii.

Kutoa huduma mbali mbali zikiwemo za ushauri wa kibiashara, msaada wa kisheria, mazingira ya upatikanaji wa taarifa muhimu, sahihi na kwa wakati katika masuala yanayohusu biashara zao, sheria, mikataba, ardhi, kodi na masuala yote yanayohusu biashara

Kuhamasisha na kusaidia wanawake walio katika Nyanja ya kiuchumi kujenga umoja na uwakilishi wao kwa lengo la kuwapa uwezo wa kuwa wajasiliamali na kutambua haki zao.

Kuwezesha mazingira ya kutambulika kwa haki za wanawake wafanyakazi na wazalishaji.

Kusaidia wanawake na wanaume wote kwa sawa katika kumiliki, kutawala, kutumia ardhi na vyanzo vingine vya uzalishaji ili kuinua maisha yao.

Kufanya utafiti katika sheria, sera na biashara /masoko kwa wanawake walio katika sekta isiyo rasmi na kuondoa (reform) sera zinazokandamiza usawa wa kijinsia.



## NINI MAANA YAA UKATILI WA KIJINSIA?

Ni kitendo chochote kinachoweza kumsababishia mtu mwingine madhara ya kimwili, kiakili au kisaikolojia. Ukatili pia unamaanisha vitendo vyenye kusudio la kulazimisha au kutisha mtu na kumpelekea kufanya jambo kinyume na matakwa yake.

## NINI MAANA YA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE?

Ni vitendo vya kumuumiza mwanamke kisaikolojia ,kimwili na kiakili kwa kumnyanyasa kwa kumzuilia/kukiuka/kumnyima haki zake akiwa katika jamii au maisha binafsi.

Viashiria vya ukatili dhidi ya Wanawake

- Kupewa nafasi za daraja la chini katika maamuzi
- Kutotambulika mchango wao katika uchumi
- Kuchukuliwa kama viumbe wadhaifu kuliko wanaume
- Kuwa wachuuzi wa biashara ndogo ndogo
- Kuwa wahanga wakuu wa aina mbalimbali za ukatili
- Kuwa na nafasi finyu katika nyanja za maendeleo
- Kutothaminiwa kazi zao
- Wanawake kubaguliwa katika nafasi za uongozi
- Kupewa thamani ndogo au kutoheshimika
- Mwanamke kupewa hadhi ya chini kutokana na mifumo mbalimbali katika jamii.

## AINA ZA UKATILI WA KIJINSIA

### Ukatili wa Kimwili

Ni kitendo anachofanyiwa mtu kinachohusisha kuumizwa mwili na huweza kuonekana moja kwa moja japokuwa wakati mwingine maumivu anaweza kuyasikia mtendewa bila mwingine kutambua kuwa amefanyiwa ukatili wa kimwili. Mifano ya ukatili kimwili ni pamoja na:

- Vipigo
- Kuchoma moto
- Matumizi ya silaha
- Kuvuta nywele
- Kusukuma
- Kunyonga mkono/mguu
- Kumpiga kichwa ukutani/sakafuni
- Kuchomwa kwa kitu chenye ncha kali sehemu yoyote ya mwili
- Kuchomwa moto
- Kunyimwa chakula
- Mtu kuhamishwa mahali bila ridhaa yake

### Ukatili wa Kisaikolojia

Ukatili wa kisaikolojia ni ukatili ambao mtu anatendewa na unamsababishia maumivu kiakili ambapo mtu mwingine hawezi kutambua kuwa mwenzake ametendewa ukatili hadi mazingira yatakapojitokeza kwa mtendewa kujieleza. Ukatili wa aina hii ni pamoja na;

- Kutukanwa
- Kufanyiwa dhihaka
- Kudhalilishwa/kuaibishwa
- Kutishiwa kuuawa,
- Wivu wa kupindukia
- Kunyimwa matunzo.
- Gubu
- Kutumiwa meseji za simu zenye vitisho au kudhalilisha

**Ukatili wa Kingono**

Ni kitendo chochote cha kujaribu kutimiza azma ya kufanya mapenzi pasipo ridhaa ya mtendewa bila kujali kuwa mtenda na mtendewa wana mahusiano au la. Kulazimishwa kunaweza kujumuisha matumizi ya nguvu/ vitisho, kutishia kutoa siri, ndoa za kulazimisha. Mifano ya ukatili huu ni pamoja na:

- Ubakaji
- Ukeketaji,
- Kushikwashikwa maungo ya mwili bila ridhaa
- Kufanyiwa upendeleo fulani kwa kulipa na tendo la ngono
- Ndoa za kulazimishwa
- Kutokuwa mwaminifu katika ndoa (Uzinzi),
- Kumwingilia mtu kinyume cha maumbile
- Kulazimishwa kufanya biashara ya ukahaba
- Usafirishaji wa wasichana au wanawake kwa ajili ya biashara ya ukahaba.





## Ukatili kiuchumi

Ukatili wa kiuchumi ni aina ya ukatili ambayo inamnyima fursa za kiuchumi mwanamke au mwanaume katika kujiongezea kipato na kuchangia katika maendeleo. Aina hii ya ukatili huwapata wanawake kutokana na hali yao ya kuwa tegemezi kwa wenzi wao. Kitendo cha kuwa tegemezi kwa wanaume kinawaathiri sana wanawake kwani hawana kauli katika mali za familia na hawashirikishwi katika maamuzi ya maendeleo. Waathirika wakubwa wa aina hii ya ukatili ni wanawake na wasichana. Mifano ya ukatili kiuchumi ni kama vile:

- Kunyang'anywa mali/mavazi,
- Kukatazwa kufanya kazi/biashara
- Ubaguzi katika ajira
- Kunyimwa kumiliki mali

- Kunyimwa haki ya kutumia mali ambayo mtu amezalisha au kumwekea masharti juu ya matumizi.
- Mtoto wa kike kunyimwa fursa ya kusoma




## JE KUNA ATHARI GANI ZA UKATILI WA KIJINSIA?

## BAADHI YA ATHARI ZA UKATILI WA KIJINSIA NI:

**Kimwili**

- Kuumia kutokana na kipigo
- Ulemavu wa kudumu
- Afya kuwa dhoofu
- Kifo

**Kingono**

- Kuenea kwa magonjwa ya zinaa
- Mimba zisizotarajiwa
- Utoaji mimba


**Kisaikolojia**

- Msongo wa mawazo
- Kushindwa kufanya biashara ipasavyo
- Kuwa na huzuni
- Kuwa na hofu /wasiwasi
- Kutokujiamini

**Kiuchumi**

- Kupoteza ajira/ biashara
- Umaskini
- Kupoteza nguvukazi ya jamii

Ukatili wa kijinsia sio suala la wanawake tu bali ni tatizo la kitaifa linaloathiri maendeleo, afya ya jamii, haki za binadamu kupunguza umasikini na kukua kwa uchumi.



Uchumi hauwezi kukua kama watu wenye uwezo wana majeraha na wamelezwa mahospitalini au wanahudumiwa majumbani. Mara nyingi suala la madhara yatokanayo na ukatili wa kijinsia tunayaangalia bila ya kuyapa uzito unaostahili bila ya kuangalia thamani ya fedha inayotumika na madhara yake kiuchumi. Tumekuwa tukiliangalia tatizo la ukatili kijinsia kwa kuangalia madhara kwa mtu binafsi, ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

## HALI YA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA SEKTA ISIYO RASMI

Tatizo la ukatili wa kijinsia limekuwa linakua na kukithiri katika sekta isiyo rasmi kwa kiasi kikubwa.

### UKATILI SEHEMU ZA KAZI:

Utafiti uliofanywa na EfG mwezi Januari,2015 katika masoko ya Ilala na Temeke unaonyesha kuwa asilimia 95.97% ya wahojiwa katika masoko yote walisema kuna ukatili dhidi ya wanawake katika masoko yao.

**Ni sehemu zipi hutumika kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia?**

- Viongozi wa mtaa,vijiji na kata
- Polisi
- Ofisi za ustawi wa jamii
- Kituo cha afya
- Vituo vya msaada wa kisheria
- Wasaidizi wa sheria(paralegal)
- Viongozi wa dini

**Ni nini cha kuzingatia kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia?**

- Kutoa taarifa mara tu unapofanyiwa kitendo cha ukatili.
- kuzingatia kutunza ushahidi .Mfano watu waliofanyiwa ukatili wa kingono hawatakiwi kuoga au kubadilisha nguo.
- Kutoa taarifa polisi
- Kwenda kupata matibabu




**ULINZI WA HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA MIKATABA YA KIMATAIFA**

Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali kuhusiana na ukatili wa kijinsia.Baadhi ya mikataba ya Kimataifa ni kama vile:

- Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948
- Mkataba wa Kimataifa wa kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake(CEDAW) wa 1979
- Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Wanawake Barani Afrika(Maputo protocal) wa mwaka 2003
- Azimio la Beijing la Masuala ya Jinsia la 1995

## 1. TAMKO LA KIMATAIFA LA HAKI ZA BINADAMU LA 1948

Usimamizi na utekelezaji wa haki na wajibu wa Haki za Binadamu vina misingi yake katika Tamko la Kimataifa la Kimataifa la Haki za Binadamu la 1948.Tamko hili lilitokana na matokeo ya Vita kuu ya Pili ya Dunia (1939 – 1945)ambayo iliambatana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Hali hii ililazimu nchi nyingi duniani kudai kuwepo kwa viwango vitakavyoongoza vitendo vya serikali kwa wananchi wake.

**Haki zilizobainishwa katika Tamko hili ni kama zifuatazo:**

- Haki  ya Usawa
- Haki ya uhuru dhidi ya ubaguzi
- Haki ya kuishi
- Haki ya uhuru na usalama wa mtu
- Haki ya uhuru dhidi ya Utumwa
- Mateso au vitendo vya Udhalilishaji
- Haki ya kutambuliwa kama mtumbele ya sheria
- Haki ya kupata msaada wa mahakama
- Uhuru wa kujieleza na kushiriki katika siasa

## 2. MKATABA WA KIMATAIFA WA KUONDOA AINA ZOTE ZA UBAGUZI DHIDI YA WANAWAKE(CEDAW) WA 1979

- Mkataba huu uliazimiwa na umoja wa Mataifa tarehe 18 Decemba mwaka 1979. Tanzania ni mojawapo ya nchi iliyoridhia mkataba huu mwaka 1985.

- Mkataba huu unaelezea vikwazo mbalimbali dhidi ya wanawake kwa kutoa mwongozo kuhusu haki sawa kwa wanawake katika nyanja za kisiasa,kijamii,fursa sawa za kielimu pamoja na uwepo wa mitaala ya elimu sawa,kuondolewa kwa ubaguzi katika ajira,malipo,pamoja na uhakika wa kuendelea na kazi katika hali ya ndoa na uzazi.

- Mkataba huu umetilia mkazo katika masuala ya kijamii hususani mahitaji na utunzaji wa watoto na wajibu wa familia,madaraka ya kikazi na maisha ya kijamii.

- Mkataba huu pia unaweka mkazo wa kuondokana na ubaguzi dhidi ya wanawake hasa hasa katika huduma za afya na uzazi.

Haki zilizotajwa katika mkataba huu zimeagiza nchi husika kuhakikisha kuwa hakuna ubaguzi dhidi ya wanawake



## 3. MKATABA WA NYONGEZA WA HAKI ZA WANAWAKE BARANI AFRIKA(MAPUTO PROTOCAL) WA MWAKA 2003

- Mkataba huu ni mkataba wa nyongeza kwa mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981.
- Mkataba huu ilitiwa saini na nchi za Umoja wa Afrika jijini Maputo, Msumbiji tarehe 11 Julai mwaka 2003.
- Tanzania imeridhia mkataba huu mnamo tarehe 3 Machi, 2007 na kukubali kama nchi kubanwa na masharti yaliyomo.
- Kwa mfumo wa Tanzania ,huwezi kumwajibisha mtu moja kwa moja au mtu kuutumia pale ambapo anaona umekiukwa.

Nchi yetu inafuata msingi kuwa sheria za kimataifa ni tofauti na sheria za kitaifa. Hivyo basi Tanzania inapaswa kuingiza mkataba huu katika sheria za nchi kwa kufanya yafuatayo:

(a) Kuingiza katika katiba ya nchi na sheria zingine

(b) Kutunga na kutekeleza sheria mahsusi na kuweka miongozo ikiwemo ile inayopinga na kukataza kabisa aina zote za ubaguzi hususani matendo yenye madhaara kwa wanawake ambayo yanahatarisha afya na ustawi wa mwanamke.

(c) Kufuata mtazamo wa kijinsia katika maamuzi ya sera, sheria, mipango ya maendeleo na sghughuli zote za maisha

(d) Kuchukua hatua za kusahihisha maeneo yote yanayoendelea na ubaguzi wa kijinsia.

(e) Kuunga mkono harakati za kuondoa ubaguzi kimataifa,kikanda na kitaifa.

## 4. HAKI ZA WANAWAKE KWA MUJIBU WA MKATABA WA MAPUTO PROTOCOL

Mkataba huu unaongelea haki za Mirathi na wajane.Mkataba wa Maputo unakomesha uonevu wa wanawake wajane katika kurithi mali baada ya mume wake kufariki.

Katika ibara ya 20 na 21 za mkataba huu zinabainisha kuwa mwanamke yeyote ana haki ya :

(a) Kutokuwekwa katika hali ya unyanyasaji,udhalilishaji na matendo ya kushushiwa hadhi.

(b) kuwa mlezi wa moja kwa moja kwa watoto wake isipokuwa tu kama ni kinyume na ustawi wa mtoto.

(c) Kuolewa tena akipenda na kwa ridhaa yake.

(d) Kurithi mali ya mume wake ikiwemo kuendelea kuishi katika nyumba ya ndoa.

(e) Kurithi katika mafungu linganifu kutoka kwa mali za wazazi wao

Mkataba huu wa Maputo unaitaka serikali kuhakikisha inatunga sheria mpya ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake.Ibara ya 3 ya mkataba huu inakataza kabisa Ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake na kuitaka Tanzania itunge sera,sheria na miongozo ya kupinga ukatili huo.

- Ibara ya 5na 8 za Mkataba huu zimeelekeza kuwa wahanga wa ukatili wa Kijinsia wapate msaada wa kisheria na pia matibabu ya kisaikolojia ili warudi katika hali ya kawaida kama awali.

## 5. AZIMIO LA BEIJING LA MASUALA YA JINSIA LA 1995

Mkutano wa beijing ulifanyika mwaka 1995 huko China.Mkutano huu ulibainisha maeneo ya kupewa kipaumbele kama vile:

(a) Kuwapatia wanawake haki ya kuwaongezea uwezo kisheria.

(b) Kuwawezesha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi

(c) Kuimarisha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini na

(d) Kuwapatia wanawake elimu,ajira na mafunzo.




S.L.P. 10618, DAR ES SALAAM
SIMU: + 255 (22) 286 3293
Baruapepe: equalityforgrowth@gmail.com
www.equalityforgrowth.org

United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

UNITED NATIONS TRUST FUND TO END VIOLENCE AGAINST WOMEN